# TIMER NATIONAL SERIES {6}
## MAJARIBIO YA MTIHANI
## DARASA LA SITA KISWAHILI

CODE0062021

Muda: Saa 1 Dak 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Mtoto ni mtoto, awe wa kike au ___1___ wote lazima waonyeshwe mapenzi na huduma kama inavyopasa. Kumdunisha mtoto wa jinsia moja ___2___ sababu ya ile ___3___ ni kukosa ___4___. Inafaa ___5___ tujue ___6___ watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ni jambo ___7___ ikiwa ___8___ pamoja na kuonyeshwa mapenzi mazuri ambayo yatawaandaa kuyajua ___9___ maishani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kijana | B. wa kiume | C. kiume | D. msichana |
| 2. | A. kuwa | B. kua | C. kuua | D. kwa |
| 3. | A. nyingine | B. lingine | C. zingine | D. mwengine |
| 4. | A. mtu | B. ubinadamu | C. binadamu | D. watu |
| 5. | A. wote | B. nyote | C. sote | D. zote |
| 6. | A. kuua | B. kwa | C. kuwa | D. kua |
| 7. | A. nzuri | B. jema | C. njema | D. mzuri |
| 8. | A. watalewa | B. wataelewa | C. watalelewa | D. watalewalewa |
| 9. | A. mengi | B. nyingi | C. mingi | D. wengi |

Kufikia darasa ___10___ sita, tumejawa na furaha kwa sababu ya bidii za walimu wetu na ___11___ pamoja ___12___ zimetufanya kutambua mambo mengi ___13___. Tumefunzwa aina za maneno kama vile ___14___ ambavyo hutoa taarifa kuhusu nomino za misamiati inayohusu sebuleni kwa mfano ___15___ ambalo ni tandiko la sakafuni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. hii ya | B. hili ya | C. hii la | D. hili la |
| 11. | A. zetu | B. zao | C. zangu | D. zake |
| 12. | A. ambayo | B. ambaye | C. ambao | D. ambazo |
| 13. | A. sanaa | B. zana | C. mno | D. kupinduka |
| 14. | A. vielezi | B. vivumishi | C. vitenzi | D. vihusishi |
| 15. | A. dari | B. shubaka | C. danka | D. zulia |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Shairi la takhmisa lina mishororo mingapi katika kila ubeti?
   A. Mitatu
   B. Miwili
   C. Minne
   D. Mitano

17. Tumia kirejeshi **'ndi'** kwa usahihi
   Mimi ______ niliyeichora picha hiyo.
   A. ndimi  B. ndiye
   C. ndio  D. ndiyo

18. Tumia sifa **'-chache'** kujazia pengo.
   Shambani kuna miti
   A. chache
   B. machache
   C. machache
   D. michache

19. Nomino **kufuli** iko katika ngeli gani?
   A. KI - VI  B. U - I
   C. LI - YA  D. A - WA

20. Wachezaji wote walivalia ______ maridadi.
   A. sare  B. majoho
   C. jezi  D. nguo

21. Andika wingi wa
   **Mwalimu aliniambia niiokote karatasi.**
   A. Walimu walituambia tuokote karatasi.
   B. Walimu walituambia tuziokote karatasi.
   C. Walimu walituambia tuziokote makaratasi.
   D. Walimu walituambia tuokote makaratasi.

22. Katika sentensi hii, kielezi ni:
   **Walimu wacheshi wameingia majilisini.**
   A. wameingia
   B. Walimu
   C. wacheshi
   D. majilisini

23. Kamilisha tashbihi:
   **Katume ni mwaminifu kama**
   A. mbwa  B. mchana
   C. kondoo  D. njiwa

24. Kitenzi **"fagia"** katika kauli ya kutendewa ni
   A. fagiliwa  B. fagiwa
   C. fagilia  D. fagia

25. Ni mmea gani huzaa kahawa?
   A. Mpareto  B. Kahawa
   C. Mbuni  D. Mpunga

26. Tumia **'amba-'** kwa usahihi
   Penseli _____ ilinunuliwa imepotea.
   A. ambazo  B. ambayo
   C. ambalo  D. ambacho

27. Chagua sentensi iliyotumia kivumishi **'-enyewe'** kwa usahihi
   A. Yai yenyewe ni jeupe.
   B. Maskanini yenyewe ni hapa.
   C. Kenge mwenyewe hutisha.
   D. Kusoma chenyewe ni kuzuri.

28. Maneno kama vile **kabla ya, kati ya** na **baada ya** huitwaje?
   A. Vivumishi
   B. Viunganishi
   C. Viwakilishi
   D. Vihusishi

29. Tumia kiunganishi sahihi kujazia pengo lifuatalo: Si vizuri kuingia darasani _____ kuubisha mlango
   A. bila  B. ili
   C. kwani  D. ila

30. Rangi ya katikati katika upinde wa mvua ni
   A. kijani
   B. samawati
   C. manjani
   D. nili

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

"Siku hazigandi." Ndivyo alivyoimba msanii mmoja wa Afrika Mashariki. Kwa hakika, hakukosea hata kidogo. Ni wachache sana ambao wana uwezo wa kuyakumbuka matukio ya siku chache tu zilizopita. Mimi namshukuru Mungu kwani, hata kama siku zimepeperuka hivyo, sijasahau yale ambayo tulifunzwa katika madarasa ya awali, kuanzia la kwanza hadi hili.

Kuhusiana na misamiati mbali mbali ambayo najivunia kuifahamu, kuna ule msamiati wa nyumbani ambao nilijifunza katika darasa la kwanza. Mwalimu Leshamta alinifahamisha mengi kama vile kiti, meza, dirisha, mlango na mengine mengi. Si hayo tu, nilijifunza mengi kuhusu shuleni ambapo, nilipata nafasi ya kutambua kuwa shuleni kuna uwanja, bendera, kengele na madarasa.

Nilipojongea hadi katika darasa la pili, Bwana Fimbocheza hakulegea bali alizidi kunifahamisha mengi kuhusu msamiati wa darasani kama vile wino, chati, rejista, kiranja na mengineyo. Nilipokaribia kukata tamaa, bwana Fimbocheza alinichangamsha kwa kunifahamisha miezi ya mwaka ambayo awali sikuwa nikijua. Nilitamani nijue kila kitu ila mwalimu alinieleza kuwa ningefunzwa baadaye.

Katika darasa la tatu, mwalimu Kaida alinifunza msamiati unaohusu sokoni. Awali, sikuwa nikijua chochote kuhusu sokoni. Baada ya wiki nzima ya mafunzo kuhusu msamiati wa sokoni, niliweza kujua mengi kama vile vibanda, wanunuzi, ratili na vichinjio. Tangu siku hiyo, nikawa naenda sokoni kila Jumamosi ili kujifunza mengi zaidi.

Niliyojifunza katika darasa la nne na la tano nayakumbuka vyema sana. Siku hazigandi. Nitakapofika katika darasa la nane, nitaweza kuyakumbuka.

---

**31.** Mwandishi anasema ni wangapi wanaweza kukumbuka yaliyopita?
A. Wadogo B. Wachache
C. Wote D. Hakuna

**32.** Kulingana na aya ya kwanza, mwandishi anamshukuru Mungu kwa kuwa
A. siku zimepeperuka
B. hakumbuki chochote
C. watu wamesahau mengi
D. anakumbuka ya awali

**33.** Ni walimu wangapi wametajwa katika ufahamu huu?
A. Watatu B. Wanne
C. Wawili D. Watano

**34.** Ni katika darasa gani ambapo mwandishi aliusoma msamiati wa darasani? La
A. kwanza B. nne
C. pili D.tatu

**35.** Ni yupi kati ya walimu hawa hajatajwa katika ufahamu?
A. Fimbocheza
B. Hedimasta
C. Kaida
D. Leshamta

**36.** Kulingana na aya tatu, mwandishi anaweza kutaja mwezi wa nane wa mwaka kuwa
A. Agosti B. Aprili
C. Juni D. Mei

**37.** Msamiati unaohusu viti milango, madirisha na meza yaliyofunzwa katika darasa gani? La
A. tatu B. nne
C. kwanza D. pili

**38.** Ni msamiati gani hapa ambao msemaji hakufunzwa katika madarasa ya awali? Wa
A. nyumbani B. sebuleni
C. shuleni D. darasani

**39.** Ni msamiati gani ambao msimulizi alifunzwa katika darasa la tano?
A. Wa nyumbani
B. Wa shuleni
C. Haukutajwa
D. Wa darasani

**40.** Ni katika darasa lipi ambapo msemaji alijifunza kuhusu rejista? La
A. tatu B. kwanza
C. pili D. nne

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Fisi na tai hula mizoga. Hawawaui wanyama kama vile simba na chui bali huwaendea wale waliojifia au waliouawa na wengine. Haimaanishi kuwa wao ni wazembe kupita kiasi. La hasha! ni jinsi yao ya kujitafutia maakuli. Ni maumbile yao.

Fisi ni mnyama mwenye sifa ya woga na ulafi. Kiboko ni mnyama mkubwa ambaye hula mimea. Kiboko ni hatari sana kwa binadamu kwa sababu anaweza kumkata mtu vipande vipande.

Ndovu wakitoka msituni na kuyavamia mashamba ya watu, wao huharibu mimea yote. Hawachagui wala hawabagui mimea iwe mihindi, migomba au mibuni, wao huharibu yote. Chui na simba nao wanaogopwa kwani wakikutana na watu au mifugo wanaweza kuwala.

Wawindaji haramu nao hushambulia ndovu na vifaru ili wazitoe pembe zao. Pembe zenyewe huthaminiwa sana. Upembe wa kifaru hutumiwa kutengenezea dawa ghali. Ngozi ya chui nayo huchunwa ili kutengenezea viatu, mikoba na mikanda ya bei za juu. Serikali imepiga marufuku uwindaji haramu ili kuwahifadhi wanyama hao ambao huwavutia sana watalii.

**41.** Ni wanyama na ndege wangapi wametajwa katika habari hii?
A. Kumi
B. Kumi na mmoja
C. Wanane
D. Saba

**42.** Badala ya kutumia neno "wazembe" mwandishi angetumia neno gani?
A. Wachoyo B. Wakali
C. Walafi D. Wavivu

**43.** Ni mnyama yupi hatari sana kwa binadamu?
A. Kiboko B. Tai
C. Fisi D. Twiga

**44.** Ukimfananisha mtu na fisi, huwa unamaanisha kuwa yeye
A. si mwoga
B. ni mlafi
C. ni mkali
D. si binadamu

**45.** Kulingana na ufahamu, ndovu huharibu mimea ifuatayo isipokuwa
A. mahindi
B. mikahawa
C. migomba
D. mihindi

**46.** Ni wanyama gani ambao huwindwa na wawindaji haramu?
A. Ndovu na tai
B. Chui na fisi
C. Viboko na vifaru
D. Tembo na vifaru

**47.** "Upembe wa kifaru" ni sawa na
A. vipusa B. kipusa
C. kichwa D. uso

**48.** Mwandishi ana maana gani anaposema "dawa ghali"?
A. Zisizo na ladha tamu
B. Ambazo si za bei rahisi
C. Za bei ya chini
D. Zile ambazo si rahisi kupata

**49.** Kulingana na ufahamu ni gani hakiwezi kuundwa kutokana na ngozi ya chui?
A. Mikoba
B. Mishipi
C. Viatu
D. Bilauri

**50.** Wanyamapori
A. huiletea nchi hasara kubwa
B. huwavutia wawindaji haramu
C. hupendwa na watalii
D. wote ni hatari kwa watu